Closing Speech During Closing Ceremony of the Conference

Dr. Khatibu Kazungu
Deputy Permanent Secretary Ministry of
Finance and Planning,
Tanzania

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo Bi. Mugabe Adam Mtani; Ndugu Kaimu Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Prof. Hozen K. Mayaya; Ndugu Kaimu Mkuu wa Chuo - Taaluma Prof. Israel B. Katega; Ndugu Makamu Mkuu wa Chuo - Mipango, Fedha na Utawala Dkt. Vedastus L. Timothy; Ndugu Washiriki wa Kongamano la Kimataifa la Mipango ya Maendeleo kutoka Tanzania na nchi za nje; Ndugu wanahabari; Mabibi na mabwana; Habari za alasiri.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa kunialika kuja kushiriki nanyi katika kulifunga kongamano hili la Kimataifa la Mipango na Maendeleo, ambalo ninaamini kwa siku zote tatu washiriki wamenufaika sana. Pili, ninapenda kukupongeza wewe na Baraza lako la Uongozi wa Chuo kwa kukisimamia vizuri Chuo chetu katika kutekeleza majukumu ya kuanzishwa kwake. Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimeendelea kutekeleza vyema majukumu yake ya kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwa mafanikio makubwa kama ambavyo Kaimu Mkuu wa Chuo alivyo nieleza punde ofisini kwake. Pamoja na changamoto kadhaa zilizopo lakini kwa kweli Chuo kinaeendelea kufanya vizuri katika nyanja zote. Sisi kama Wizara tunajivunia mno taasisi hii. Hongera sana Makamu Mwenyekiti kwa usimamizi mzuri.

© IRDP, 2018 *ISBN 978-9976-9974-0-8*

Pia, napenda kutumia fursa hii kuupongeza Uongozi wa Chuo chini ya Kaimu Mkuu wa Chuo Prof. Hozen K. Mayaya kwa kuandaa Kongamano hili la Kimataifa la Mipango na Maendeleo lililojikita kwenye kutafuta njia na mbinu za kudumu za kuwashirikisha wananchi wa Vijijini katika nchi zinazoendelea kuwa washiriki hai wa ujenzi wa uchumi wa viwanda. Hongereni sana.

Nimefurahi kuelezwa kuwa Kongamano hili limewaleta kwa pamoja washiriki kutoka nchi zinazoendelea na zilizoendelea. Ni imani yangu kuwa kongamano hili limekuwa darasa tosha kwa wahadhiri, watafiti, watunga sera, watekelezaji wa Mipango ya Maendeleo, wanazuoni na wadau wa masuala ya Mipango ya Maendeleo.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, nadhani utakubaliana nami kuwa masuala ya ujenzi wa uchumi wa aina yoyote unategemea sana ushirikiano wa wadau mbalimbali ndani ya nchi husika na nje ya nchi. Hivyo, uwepo wa washiriki kutoka nje ya Tanzania ni kielelezo tosha kuwa agenda za Kongamano hili zimekuja kwa wakati kwa vile zinagusa maisha ya wananchi wa kawaida waliopo Vijijini na ambao ni wengi na kwa mazingira ya nchi nyingi zinazoendelea wameendelea kujiona hawashirikishwi. Lakini ukweli ni kwamba Serikali yetu tangu Awamu ya Kwanza chini ya Baba wa Taifa Hayati Mwl. J.K. Nyerere alijikita katika kuwashirikisha wananchi wa Vijijini katika kujiletea maendeleo yao. Uanzishaji wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ni ushahidi wa hili. Chuo hiki kilianzishwa mahususi kwa ajili ya kuwaandaa wataalamu wa kupanga, kusimamia, kutekeleza na kutathimini mipango ya maendeleo, hasa maendeleo Vijijini.

© IRDP, 2018 *ISBN 978-9976-9974-0-8*

Ushahidi mwingine ni uanzishaji wa Shirika la Viwanda Vidogovidogo (SIDO) ambapo wananchi wengi Vijijini waliwezeshwa katika kuendeleza ujuzi wao wa utekelezaji wa bidhaa mbalimbali. Hivyo, sisi Tanzania tuna uzoefu wa kutosha wa kuwashirikisha wananchi wa Vijijini katika masuala ya Uchumi na hususani Uchumi na Viwanda.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, ninatambua pia kwa sasa watu wana mjadala mpana juu ya kiwanda ni nini. Kwa tafisiri pana viwanda ni mahali ambapo shughuli za kiuchumi zinafanyika, malighafi zinachakatwa na kubadilishwa kuwa bidhaa kwa msingi wa kuongeza thamani. Hivyo, Serikali ya awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inaposema inataka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo 2025 inakusudia kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa kutumia rasilimali zilizopo na hivyo kupanua dhana ya viwanda. Dhana ya viwanda tuliyo nayo ni shughuli yoyote ya uongezaji thamani ya bidhaa. Hili halikuibuka hivihivi tu. Bali linatokana na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 - 2012/21 unaojikita katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Historia ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda katika nchi yetu sote tunaijua. Tunajua wapi tulipatia na wapi tulikosea. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, msisitizo upo kwenye kutengeneza mazingira rafiki na wezeshi ya kufufua viwanda vilivyokufa na kuanzisha viwanda vipya. Suala la uchumi wa viwanda ni suala ambalo halikwepeki kwetu Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea. Ni kupitia uchumi wa viwanda, nchi yetu itaweza kuleta mageuzi ya haraka na kujenga misingi imara ya Uchumi. Hata hivyo,

© IRDP, 2018 *ISBN 978-9976-9974-0-8*

kufanikiwa huko kutategema mambo kadhaa. Mambo hayo ni pamoja na utashi, uzalendo, uadilifu na utaifa. Ni jukumu la kila mtanzania na mwananchi yeyote kutoka nchi zinazoendelea kuzingatia haya. Hivyo, nitoe wito kwamba kila mtanzania kwa nafasi yake awe mzalendo kwa nchi yake, awe mwadilifu kwa Taifa lake na pia achangamkie fursa ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuanzisha kiwanda chochote kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, nimefurahi kusikia pia kuwa moja ya mada ilikuwa juu ya Nafasi ya Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kukuza viwanda Tanzania (The Role of Public - Private Partnership in Promoting Industrialization in Tanzania). Mada hii kama zilivyo mada nyingine ambazo sikuzitaja imekuja kwa wakati kwani ina sadifu mazingira ya sasa ya ujenzi wa Uchumi wa Viwanda. Mheshimiwa Waziri Viwanda, Biashara, na Uwekezaji katika hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2017/18 alipokuwa anazungumzia umuhimu wa sekta binafsi katika uchumi wa viwanda, alisema Nanukuu *"Kimsingi, sekta binafsi inajumuisha shughuli zote za uzalishaji kiuchumi zinazoendeshwa na watu binafsi, makampuni, taasisi pamoja na shughuli zinazohusisha ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (Joint Ventures). Kwa maneno mengine, sekta binasi inajumuisha jasiriamali ndogondogo sana, ndogo na za kati (Micro, Small and Medium Enterprises - MSHEs) ambazo uzoefu duniani unaonesha ndizo zenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii"*. Mwisho wa kunukuu.

Kwa mantiki hiyo, ushirikishwaji wa wananchi wa Vijijini ambao wengi wao wameangukia kwenye jasiriamali ndogondogo sana na ndogo (yaani Micro and Small Enterprises) ni jambo la msingi sana. Jukumu letu kama Serikali na pia Wizara

© IRDP, 2018 *ISBN 978-9976-9974-0-8*

inayohusika katika kutoa fedha za maendeleo ni kuendeleza na kuboresha mazingira ya watu wote Mijini na Vijijini, wafanya biashara wakubwa na wadogo kushiriki katika ujenzi wa Uchumi wa Viwanda kwa faida ya Taifa lao.

Ndugu Makamu Mwenyekiti wa Baraza, naomba kumaliza kwa kutoa ahadi kwamba Wizara itaendelea kuwa karibu na Chuo kwa kukitumia katika masuala mbalimbali ya utaalamu wa Mipango. Tunajua Chuo kina hazina kubwa ya wataalamu wa mipango nchini na wenye kutumia uzoefu na weledi mkubwa. Aidha, tutahakikisha makongamano kama haya yanaendelea kufanyika hapa chuoni kwa vile yanaleta chachu mpya ya kufikiri na kuja na mbinu mpya shirikishi. Ujenzi wa Uchumi na Viwanda ni kazi ngumu inayohitaji ushiriki wa kila mtu, makundi mbalimbali ya watu, na taasisi za utafiti na za elimu ya juu kama Chuo cha Mipango ya maendeleo Vijijini .

Ushauri wangu kwenu ni kwamba , kupitia jukwaa hili Chuo kianzishe au kiimarishe mahusiano na ushirikiano na taasisi za ndani na nje kwa kuendesha mafunzo ya muda mrefu, mafunzo ya muda mfupi, tafiti na shughuli za ushauri na uelekezi katika nyanja mtambuka za mipango na maendeleo. Njia hii itawezesha Chuo kupata uzoefu na kujijengea uwezo kutoka kwa vyuo washirika. Sisi kama wizara mama tutakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalamu na kiutawala ilikufanikisha adhima hii.

Ndugu Makamu Mwenyekiti, mwisho napenda kurudia tena kukushukuru kwa kunialika kuja kufunga kongamano hili. Nilitamani kuwa nanyi tangu siku ya kwanza, lakini kutokana na majukumu ya Bajeti Kuu nilishindwa. Hata hivyo ninaahidi kushirikiana nanyi siku nyingine katika shughuli nyingine. Aidha,

© IRDP, 2018 *ISBN 978-9976-9974-0-8*

ninawatakia safari njema ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na pia safari njema wakati wa kurudi kwenu. Baada ya kusema hayo ninatamka kwamba Kongamano la Kimataifa la Mipango na Maendeleo 2018 limefungwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

© IRDP, 2018 ***ISBN 978-9976-9974-0-8***